

MFUMO>> Unasaidia kuokoa muda na fedha kwa mwananchi

e-GA kuendelea kusimamia matumizi TEHAMA serikalini

Na MWANDISHI WETU

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba, amesema mamlaka hiyo itaendelea kusimamia matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) serikalini.

Amesema lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha yanaleta tija kwa kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kurahisisha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi, kwa wakati mahali walipo.

Kauli hiyo aliitoa alipozungumzia kuhusu matumizi ya mfumo wa TEHAMA serikalini.

"Miongoni mwa eneo ambalo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan analipa kipaumbele ni kuimarisha Serikali Mtandao kwa kuhakikisha taasisi za umma zinatumia TEHAMA katika utendaji kazi wake na wananchi wanapata huduma za serikali kidijitali mahali popote na muda wote.

"Katika kuhakikisha tunafikia lengo la Rais, e-GA kwa kushirikiana na taasisi nyingine za umma tumetengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA ambayo imesaidia kupunguza gharama, kuokoa muda, kuongeza ufanisi na kuwarahisisha wananchi kupata huduma za serikali kidijitali mahali walipo," alisema

Akizungumzia mfumo wa e-Mrejesho, Mhandisi Ndomba alisema unawawezesha wananchi kutuma kero au malalamiko, maoni, maswali na pongezi kidijitali kwenda taasisi yoyote ya umma, kisha kupata mrejesho wa utekelezaji wake kidijitali mahali walipo.

Pia, unasaidia kuokoa muda na fedha kwa kuwa mwananchi halazimiki kusafiri umbali mrefu kwenda ofisi ya umma kuwasilisha malalamiko yake au kufuatilia utekelezaji wake, badala yake anafanya hivyo kidijitali kupitia simu ya kiganjani mahali alipo.

"Zamani ilikuwa mtu akihitaji kutoa maoni au malalamiko kuhusu huduma inayotolewa na taasisi ya umma ilimlazimu kufika katika taasisi hiyo na kuwasilisha malalamiko yake katika sanduku la maoni au barua, kisha kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji, lakini hivi sasa anawasilisha maoni hayo kidijitali," alisema.

Alieleza mfumo wa e-Mrejesho unapatikana kwa njia tatu ambazo ni kupitia simu ya mkononi kwa kubofya *152*00#, kisha kuchagua namba 9 na namba 2. Njia zingine ni kupitia simu janja kwa kupakua aplikesheni (Mobile App) ya e-Mrejesho inayopatikana katika 'Play Store' na Apple App Store na nia ya Tovuti ya e-mrejesho.

gov.go.tz.

Aliongeza ikiwa mwananchi atakosea kuwasilisha lalamiko lake katika taasisi husika, mfumo wa e-Mrejesho unaruhusu lalamiko kuhamishwa kutoka taasisi moja kwenda nyingine, pia unamruhusu mwananchi kukata rufani kwenda ngazi ya juu ya taasisi ikiwa hatoridhika na majibu yaliyotolewa kuhusu lalamiko lake.

"Mfumo huu unasaidia kuongeza uwajibikaji, kwa kuwa lalamiko linapofika katika taasisi litaonekana ngazi zote za uongozi wa taasisi hiyo na kila ofisa aliyelifungua ama kulifanyia kazi ataonekana, pia mfumo unafanya uchambuzi wa taarifa na kumuwezesha Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Utumishi na Katibu Mkuu Kiongozi kuona malalamiko yaliyowazi, yanayoshugulikiwa na yaliyokamilika kupitia 'dashboard' maalumu," alisema.

Katika kuhakikisha mifumo ya TEHAMA serikalini inawasiliana na kubadilisha taarifa, Mhandisi Ndomba alibainisha mfumo wa e-Mrejesho unao uwezo wa kubadilishana taarifa na mifumo mingine kupitia Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (GovESB) na tayari mifumo imeunganishwa na e-Mrejesho kupitia mfumo wa GovESB.

Mfumo wa e-Mrejesho umetengenezwa

na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zote za umma zimeunganishwa.

Machi 13, mwaka huu, Rais Dk. Samia aliwataka viongozi wa umma kutumia mfumo wa kielektroniki wa mawasiliano wa e-Mrejesho kupokea maoni ya wananchi kuhusu serikali na kutoa mrejesho kwa wananchi kupitia mfumo huo.

Dk. Samia alitoa maelekezo hayo Ikulu, jijini Dar es Salaam, baada ya kuwaapisha viongozi aliowateua katika nafasi mbalimbali wakiwemo wakuu wa mikoa, katibu mkuu, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa Halmashauri.

Alisema viongozi wa umma wanapaswa kufahamu na kutumia mifumo ya TEHAMA iliyopo serikalini katika utekelezaji wa majukumu yao, ikiwemo kutumia mfumo wa e-Mrejesho kupokea maoni ya wananchi na kutoa mrejesho kwa wananchi na serikali kuhusu utekelezaji wa maoni hayo.

"Nendeni mkatumie mfumo wa e-Mrejesho nyie mpate mrejesho na sisi tupokee mrejesho, lakini na wananchi wapate taarifa kupitia huu mfumo, ndivyo tutakavyofanya kazi kwa haraka na kwa ufanisi zaidi tukitumia mifumo," alisisitiza.